

## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI MBEYA

Simu: +255- 0252504298  
Fax: +255-0252503492  
Barua pepe:  
[mbeyauwsa@mbeyauwsa.or.tz](mailto:mbeyauwsa@mbeyauwsa.or.tz)



S.L.P 2932  
MBEYA

### MAMBO YANAYOSABABISHA ANKARA ZA MAJI KUWA KUBWA

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka mjini Mbeya UWSA imegundua malalamiko mengi ya wateja yanayohusu bili (Ankara) zao kuwa kubwa. Baada ya uchunguzi imegundulika kuwa ongezeko la bili za wateja linasababishwa na.

- Bomba linalodondosha maji kwa matone matone mfululizo.
- Maji yanayovuja katika mtandao wa mabomba ya ndani (Internal Plumbing System).
- Maji yanayotiririka mfululizo kutokana na kuharibika kwa boya la choo cha kuvuta.
- Kufua kwenye bomba na maji yakiwa yanaendelea kutiririka.
- Kupiga mswaki huku bomba la maji likiwa linaendelea kutoa maji. -watoto wafundishwe matumizi mazuri ya maji.
- Kutumia majisafi na salama kwa ajili ya kumwagilia bustani, maji ya umwagiliaji si rahisi kuyakadiria; inashauriwa kutumia kutumia ndoo kumwagilia (Watering can)
- Kuosha vyombo wakati maji yanaendelea kutiririka. Ni vyema kuchota maji na kuosha pembeni.



Unashauriwa kuchota maji kwenye beseni na kuoshea vyombo badala ya kutumia maji ya bombani moja kwa moja

Umwagiliaji maji shamba la miti kwa kutumia mpira husababisha matumzi makubwa ya maji na bili ya maji kuwa kubwa. Tumia ndoo au watering can



Umwagiliaji wa bustani kwa kutumia mpira husababisha mengi kutumika na kukusababishia bili kbuwa yamaji Tumia Watering can au ndoo kumwagilia

weka utaratibu wa kusoma na kuchunguza mita yako ya maji iwapo mishale ya mita inazunguka wakati mabomba yakiwa yamefungwa ni dalili kuwa kuna mvujo na maji hayo yataongeza bili yako ya maji ambayo utalazimika kuilipia. Ukiona hali hii wasilianana na kitengo cha Huduma kwa wateja au piga simu 0800780050 (bure) kwa uchunguzi na ushauri.

“Maji kwa uhai: Water for life”

Imetayarishwa na :  
Ofisi ya Uhusiano  
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA  
MBEYA